

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

Zanzibar  
30 Agosti, 2023

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uhamisho na uteuzi wa viongozi kama ifuatavyo:

**A. Uhamisho wa Naibu Mawaziri**

- i. Mhe. David Ernest Silinde amehamishwa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenda kuwa Naibu Waziri wa Kilimo na Mhe. Alexander Pastory Mnyeti atakuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**B. Uteuzi wa Katibu Mkuu**

Amemteua Balozi Mhandisi Aisha Amour kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi.

**C. Uteuzi wa Wajumbe wa Wizara ya Mipango**

Kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 5 (1) (c) cha Sheria ya Tume ya Mipango Na. 1 ya mwaka 2023 amewateua wafuatao kuwa wajumbe wa Tume ya Mipango:

- 1) Balozi Ombeni Yohana Sefue – Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu
- 2) Bw. Omar Issa – Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO na Mkuu wa Chuo cha Nelson Mandela.
- 3) Balozi Ami Ramadhan Mpungwe – Balozi Mstaafu na Mjasiriamali.
- 4) Bi. Maryam Salim – Meneja Mkazi wa Benki ya Dunia nchini Cambodia.

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

